**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**MKOA WA KATAVI**

Telegraphic: ***"REGCOM"***
Simu/Fax: *025-2957108*
*E-mail:ras.katavi@tamisemi.go.tz*

**OFISI YA MKUU WA MKOA,**
S. L. P. 235,
**MPANDA - KATAVI.**

10 Juni, 2020

# TANGAZO LA KUUZA MAZAO YA MSITU (SLIPA) KWA NJIA YA MNADA

1. Katibu Tawala wa Mkoa wa Katavi anatarajia kuuza mazao ya misitu **(slipa 3,562)** za mti aina ya Mkurungu kwa njia ya mnada ambayo yamehifadhiwa ndani ya Msitu wa Hifadhi ya Tongwe Mashariki katika eneo la Nguye lililopo umbali wa Kilometa 16 kutoka Barabara Kuu ya Mpanda – Kigoma.
2. Mnada utafanyika tarehe 20 hadi 21 Juni, 2020 katika eneo ambako mazao yamehifadhiwa ndani ya Msitu wa Hifadhi. Mnunuzi atatakiwa kufika katika eneo la Mnada akiwa na nakala ya Kitambulisho cha Mpiga Kura au Kitambulisho cha Taifa au Nakala yenye Taarifa za Kampuni anayoiwakilisha.
3. Mazao (Slipa) yatauzwa kwa ujazo ($m^3$) na kama yalivyo kwa kila Loti na Mnunuzi atakayeshinda hatakuwa na haki ya kudai fidia. Baada ya mauzo mnunuzi atawajibika kulinda mazao aliyonunua.
4. Mnada utaendeshwa kwa kuzingatia kifungu namba 94(3) na (4) cha Sheria ya Misitu Na. 14 ya mwaka 2002 kikisomwa pamoja na Kanuni ya 31(b) ya Kanuni za Sheria ya misitu za mwaka 2004.
5. Mnada utafanyika hadharani wakiwepo wanunuzi wote katika eneo yalipohifadhiwa mazao.
6. Wanunuzi wanakaribishwa kutembelea na kukagua mazao hayo wakati wa saa za kazi kuanzia saa mbili (2:00) asubuhi hadi saa tisa na nusu (9:30) alasiri siku ya tarehe 14 na 15 Juni, 2020 katika eneo yalipohifadhiwa. Wasiliana na Katibu

Tawala wa Mkoa kupitia Afisa Misitu kwa namba 0786 881 155 kwa msaada wa kutembelea na kukagua mazao hayo.

7. Wanunuzi watatakiwa kujiorodhesha kwenye Ofisi ya Katibu Tawala wa Mkoa kabla ya kwenda kukagua mazao hayo.
8. Mnunuzi atakayeshinda atatakiwa kulipia asilimia ishirini na tano (25%) ya thamani yote ya Loti ndani ya siku tatu (3) baada ya kushinda na fedha hizo hazitarudishwa. Asilimia sabini na tano (75%) iliyobaki italipwa ndani ya siku kumi na nne (14) baada ya mnada. Malipo yote yatafanyika kwenye akaunti ya benki ambayo itatolewa na Katibu Tawala wa Mkoa wa Katavi.

Imetolewa na;

Abdallah M. Malela
**Katibu Tawala wa Mkoa**
**KATAVI.**

**10 JUNI, 2020**